HEALTH PROMOTION TANZANIA

# Mahudhurio ya Wanaume kwenye Huduma za Afya ya Uzazi huboresha Afya ya Mama na Mtoto

Toleo Na. HDT/2014/001

5 Februari 2014

*Ushiriki wa wanaume katika huduma za afya ya uzazi ni jambo la muhimu sana na linawekewa msisitizo na sera ya afya na mikakati yake. Umuhimu wake ni kama vile:*

- *afya ya mama wakati wa ujauzito huwa bora kwani mwanaume anakuwa mstari wa mbele kumpeleka mwenza wake hospitali pindi anapoona dalili za hatari,*
- *mama kupata msaada wa mwenzi wake na kufanya maandalizi muhimu kwa ajili ya kujifungua ikiwemo kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya mahitaji siku ya kujifungua na baada ya hapo,*
- *afya ya mama kuwa bora kwa kuwa atakuwa na muda wa kupumzika baada ya uzazi mmoja na mwengine kwa wote kuelewa umuhimu wa kupanga uzazi na kukubaliana njia ya kutumia;*
- *afya ya familia nzima kuwa bora kwa kwasababu maamuzi mengi ya afya ya familia hufanywa na wanaume kama vile utayari wa kupata huduma za afya, uhiari wa kupima afya, kupata matibabu na gharama zake.*



Kuna jitihada nyingi za kumshirikisha mwanaume katika masuala ya afya ya uzazi zinayofanywa na serikali na mashirika binafsi ya kitaifa na kimataifa ikiwemo kupanga mikakati na sera zitakazoshawishi na kuvutia wanaume kufika katika hospitali na vituo vya afya ili kupata huduma za afya ya uzazi au kusindikiza wenza wao katika kliniki za awali na baada ya ujauzito.

Moja kati ya mikakati kuhusu suala la kumshirikisha mwanaume katika afya ya uzazi ni ***kuanzishwa kwa huduma rafiki kwa wanaume wanaofika katika hospitali na vituo vya afya,*** mkakati unaotekelezwa na kusimamiwa na shirika la kimarekani la Engenderhealth chini ya mradi wa CHAMPION. Shirika hili limeweza kusaidia hospitali mbalimbali nchini Tanzania kutekeleza mkakati huu wa kumshirikisha mwanaume katika afya ya uzazi. Huduma hizi ni pamoja na kutoa kipaumbele cha huduma kwa wenzi waliohudhuria pamoja na motisha nyingine zinazobuniwa katika eneo husika.



*Picha kwa Hisani ya:* ***MoHSW***

Pamoja na jitihada hizi, imeonekana kuwa, baadhi ya wanaume bado hawana taarifa kuhusiana na ushiriki wa wanaume katika masuala ya afya ya uzazi. Hili limeonekana katika tamasha la jinsia lililofanyika mwezi wa Septemba 2013 kuanzia tarehe 3 hadi 6 katika viwanja vya Asasi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Mabibo Dar es Salaam. Kwenye majadiliano na wanawake wanaharakati toka mikoani waliohudhuria tamasha hilo, walielezea jinsi wanawake wanavyonyanyasika hata katika kipindi cha ujauzito na kunyonyesha.

Maelezo yalionyesha kuwa, 80% ya wanawake waliohojiwa wamewahi kupata manyanyaso ya aina mbalimbali na hata kupigwa wakiwa wajawazito au wananyonyesha. Hii inadhihirisha kuwa, ufahamu ama uelewa kuhusu afya ya uzazi ni mdogo kwa wanaume. Msisitizo ulitolewa na wanawake hao kuhusu umuhimu wa kuongeza jitihada za kuelimisha wanaume ili wafuatilie afya za wenza wao, pia wanaume wenyewe wapende kujihusisha na masuala ya afya ya uzazi ikiwa ni pamoja na kwenda na wake zao kupata huduma hizo.


Ushiriki wa wanaume kwenye huduma za afya ya uzazi hujenga upendo na ubora wa familia. Mahojiano yalifanyika kwa wanaume waliohudhuria huduma za afya ya uzazi wakiwa na wenzi wao katika hospitali ya Sinza Palestina jijini Dar es Salaam ambayo ni mojawapo katika wilaya ya Kinondoni inayotoa huduma hii kwa majaribio (piloting). Wanaume wengi walionyesha kuvutiwa na huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo kwa kumpa kipaumbele mama anayeambatana na mwenzi wake. Vilevile wanaume hao walikiri kuwa, uelewa juu ya afya za wenzi wao umeongezeka na afya zao kuimarika kwa kusimamia matumizi sahihi ya dawa na maelekezo yanayotolewa na wahudumu wa afya. Kuhusu matayarisho ya kujifungua, wanaume wamekiri kutambua umuhimu wa kununua vifaa na nguo kwa ajili ya maandalizi ya mtoto tofauti na awali walipokuwa wakiambiwa kununua nguo wanaona ni jambo lisilo na umuhimu.

Mradi huu wa CHAMPION pia ulianzisha na kusimamia mtandao unaoitwa MenEngage Tanzania (MET). Mtandao huu unaundwa na asasi zinazojihusisha na miradi mbalimbali ya kuboresha afya kwa kuzingatia kijinsia. CHAMPION kwa kusaidiana na mtandao huu, hubaini maeneo yanayohitaji ushawishi wa sera na maadili ili kuboresha afya ya jamii. Shirika la Health Promotion Tanzania (HDT) ni mwanachama wa mtandao huu na linachukua fursa hii kuhamasisha wanaume kushiriki kikamilifu katika huduma za afya ya uzazi ili kujenga familia bora na yenye afya. Vifo vingi vya uzazi hutokea kutokana na kuchelewa kwa mama kupata huduma katika kituo cha afya, lishe duni wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua. Kama mwanaume atashiriki kikamilifu na kufuatilia huduma na maelekezo ya afya ya mwenzi wake, vifo vingi vitaepushwa.

*Mradi wa **CHAMPION** ni mradi unaotekelezwa na shirika la Engenderhealth Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani linaloshirikisha wanaume katika masuala ya afya ya uzazi. Mradi huu unatekelezwa katika wilaya 42 kwenye mikoa 15 ili kufikia wanaume walio na umri zaidi ya miaka 25, wanawake na vijana.*

*Mtandao wa MenEngage Tanzania, ni sehemu ya ushirikiano wa kidunia unaojihusisha na utetezi kwa kushirikisha wanaume na vijana ili kupunguza tofauti za kijinsia na kuimarisha afya za wanawake, wanaume, wasichana na wavulana. Mtandao huu una wajumbe 21 wanaowakilisha serikali ya Tanzania, mashirika ya kimataifa na yale ya kitaifa. Lengo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya na kuboresha ushiriki wa wanaume katika huduma za afya wanaume ili kuzuia maambukizi ya VVU na kuboresha matokeo ya afya ya uzazi.*

**MIHIMILI YA HDT**




**Kwa taarifa zaidi wasiliana na: programs@hdt.or.tz**

**HEALTH PROMOTION TANZANIA [HDT]**

**MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM**

Jengo la Josam Ghorofa ya Kwanza,
16 Mikocheni B,
Barabara ya Coca Cola,
S.L.P. 65147 Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 (0)22 27772264
Nukushi: +255 (0) 22 2772299